



DOUBLE MERIT INTERNAL EVALUATION

EARLY YEAR'S ASSESSMENT

SN:T17P7

GRADE 5 - 2021

SHUGHULI ZA KISWAHILI

JINA:.....

NAMBARI YAMWANAFUNZI

JINSIA:

MVULANA

MSICHANA

JINA LA KAUNTI:.....MSIMBO WA KAUNTI

JINA LA KAUNTI NDOGO:.....MSIMBO WA KAUNTI NDOGO

JINA LA SHULE:.....MSIMBO WA SHULE

JEDWALI LA ALAMA

VIWANGO VYA KUTATHMINI

	KUZIDISHA MATARAJIO	KUFIKIA MATARAJIO	KUKAROBIA MATARAJIO	MBALI NA MATARAJIO
KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA	5	4	3	0 - 2
KUSOMA KWA SAUTI	90 na Zaidi	50 - 89.	10 - 49	0 - 9
UFAHAMU	5	4	3	0 - 2
SARUFI	17- 20	10- 16	6 - 9	0 - 5

SN:T17P7

KISWAHILI GREDI YA TANO

Msikilize mwalimu akisoma kifungu kisha ujibu maswali (Alama 5)

Pendo ni mwanafunzi wa gredi ya tano Anaishi katika kisiwa cha Tanga. Kisiwa hicho kina watu wengi sana. Yeye hupenda somo la kiswahili. Somo hilo analipenda kwa sababu linafunzwa vizuri na mwalimu wao.

Kila siku kabla ya somo wao husikiliza hadithi kwenye rununu ya mwalimu wao. Mwalimu wao huwaandaa kabla ya kipindi na kuwauliza maswali mepesi mepesi yanayotokana na hadithi ya rununu.

Pendo hufurahishwa sana na hadithi hizi za rununu zenye burudani na maadili. Nyumbani Pendo hutazama vibonzo kwenye runinga kipakatalishi. Pia husoma vitabu vya hadithi fupifupi na kujifunza msamiati mbalimbali. Kutokana na bidii zake Pendo amekuwa msemaji bora wa kiswahili na kupata uwezo mzuri wa kukariri mashairi na kushiriki michezo ya kuigiza.

(i) Pendo ni mwanafunzi wa gredi ya

(ii) Pendo anaishi wapi ?

_____ (alama 1)

(iii) Kabla ya kuanza somo la kiswahili wanafunzi husikiliza hadithi kwenye

(iv) Pendo akiwa nyumbani hutazama nini?

(v) Kutokana na bidii zake Pendo amekuwa

KUSOMA KWA SAUTI (Alama 10)

Soma kwa sauti ufahamu huu

Upendo ni hali ya kuvutwa au kuingiwa moyoni na mtu au kitu. Hali ya upendo huanzia na wazazi kwa mtoto. Mtoto anapozaliwa wazazi humwonyesha upendo wao katika juhudi zao za kuhakikisha amepewa lise bora na kulazwa mahali pazuri. Pia humnunulia nguo na vifaa vya kuchezea.

Hali hiyo ya upendo pia hudhirika kwa ndugu zake wanapopewa haki zao bila ya kudhulumiwa. Kwa hivyo wazazi ni watu ambao wanastahili kupewa heshima kwa kukupa msingi bora wa maisha. Ni vyema kila unapoamka asubuhi kuwasalimu wazazi wako na ndugu zako. Unapofanya hivyo utakuwa ukionyesha upendo kwao.

Kumbuka upendo ni nguzo muhimu katika maisha mazuri ya nchi yetu tukufu ya Kenya.

SEHEMU YA B: SARUFI (Alama 20)

1. Pigia mstari kulingana na maagizo mabanoni

(i) Kamau alienda kanisani (Nomino ya pekee) (al 1).

(ii) Mama amenunua chumvi (Nomino ya wingi) (alama 1)

(iii) Kuchora kunafurahisha (Nomino ya kitenzi jina) (al 1)

2. Badili nomino hizi katika umoja au wingi

Umoja

Wingi

(a) Ukuta _____

(b) Ndizi _____

(c) Magonjwa _____

3. Bangili huvaliwa mkononi ilhali _____ huvaliwa masikioni (kipini, herini) (alama 1)

4. Andika sentensi ifuatayo kwa herufi kubwa
Fatuma alienda Mombasa ijumaa, (alama 1)

5. Tegua vitendawili vifuatavyo. (alama 2)

(a) Dhahabu yangu ya thamani haisimami _____

(b) Mama nieleke _____

6. (a) Andika saa 7.15 kwa maneno. _____ (alama 1)

1) (b) Kengele ya chamcha hugongwa wakati gani? (alama 1)

7. Kamilisha methali zifuatazo.

(a) Mtaka cha mvunguni sharti _____ (alama 1)

(b) Atangaye sana na jua (alama 1)

8. Idadi ya silabi katika mshororo wa shairi huitwa _____

(mizani, vina, ubeti) (alama 1)

9. Pigia mstari msamiati wa hospitali pekee

(kipimajoto, machela, sebule, kipakatalishi, parachichi)

10. Kamilisha sentensi zifuatazo

i) Baba aliwaingiza ng'ombe kwenye (sisi, zizi)

(ii) Juma ali _____ nguo kwa sabuni (vua, fua) (alama 1)

11. Taja vinyume vya maneno yafuatayo

(i) cheka _____ (alama 1)

(ii) lala _____ (alama 1)

C: UFAHAMU (Alama 10)

Soma ufahamu ufuatao kisha uyajibu maswali.

Hapo zamani za kale paliishi msichana mmoja kwa jina chaurembo. Alikuwa msichana aliyeumbwa akaumbika. Alikuwa malaika. Chaurembo alikuwa na urembo ule wa kipekee. Alipenda mtindo na kufurahia mada ya mapambo wakati wa somo la Kiswahili.

Mwalimu aliwafunza mapambo kama vile herini, vipini, bangili na mkufu. Chaurembo alikuwa msichana mwenye bidii kama zile za mchwa na mwenye nidhamu wa kupigiwa mfano na kila mtu. Aliamini kuwa heshima si utumwa.

Familia yake iliishi maisha ya umaskini wazazi wake walimuhimiza kila siku awe mwenye heshima na bidii masomoni. Pia alifahamu kuwa maishani lazima angemjua Mungu na kumwomba ili afaulu.

a) Msichana anayetajwa katika ufahamu anaitwaje?
_____ (alama 1)

(b) Taja mapambo mawili yaliyozungumziwa kwenye ufahamu _____ na _____ (al 1)

(c) Kamilisha methali ifuatayo: heshima si _____ (alama 1)

(d) Familia ya Chaurembo iliishi maisha gani? _____ (alama 1)

SEHEMU YA E: KUANDIKA

Andika insha ya kulisimua kuhusu;

MCHEZO NIUPENDAO
